

# Uhusiano wa hali ya hewa na maisha ya kiroho

Mkusanyiko wa vifungu nya Biblia vinavyokumbusha hali ya hewa, majadiliano ya kitheolojia, maisha ya kiroho, maombi na nyimbo. Kimeandaliwa na wajumbe wa Umoja wa Makanisa ya Kiinjili katika mabara matatu ya Ulaya, Afrika na Asia (UEM).



„Amani duniani“



Dr Jochen Motte, Longgena Ginting, Richard Madete, Katja Breyer (kutoka kushoto)

*"Muda nchi idumupo, majira ya kupanda, na mavuno, wakati wa baridi na wakati wa hari, wakati wa kaskazi na wakati wa kusi, mchana na usiku havitakoma"* (Mwanzo 8:22). Kufuatana na ahadi hii ya Mungu, Umoja wa Makanisa ya Kiinjili (UEM) tangu 2008, umekuwa ukielimisha makanisa yake kwa njia ya maonyesho na miradi mbalimbali ikihamasisha kwamba, si jukumu la mwanadamu kuiharibu dunia. Mungu ametoa dunia hii kwa wanadamu kama mahali pa kuishi na inapaswa kutunzwa.

Leo, mabadiliko ya hali ya hewa na uharibifu wa mazingira ni tishio kubwa kwa wanadamu na kwa mazingira. Makanisa ndani ya UEM katika Afrika, Asia na Ujerumania yameitikia changamoto hii kwa kuweka mikakati katika kukabiliana na mabadiliko haya katika miradi mbalimbali ya mazingira, uelimishaji na uhamasishaji.

UEM inajumuika pamoja na makanisa ulimwenguni kote, katika mpango wa "Amani Duniani". Kwa njia ya kutembeleana, wajumbe wa makanisa ya UEM wanatiana nguvu katika kupiga vita dhidi ya uharibifu wa misitu, uporaji wa ardhi na uharibifu wa mazingira unaosababishwa na uchimbaji wa madini, ulimaji mkubwa wa michikichi, pamoja na uchafuzi wa mazingira mijini.

Zaidi ya hayo, makanisa yameanza kutumia theolojia ya uumbaji kufuatana na mila na desturi za watu katika majimbo haya matatu. Hali ya hewa na uasilia wake vinahusishwa na maneno ya Biblia, mahojiano ya theolojia, maisha ya kiroho ya watu, sala na uchukua ji wa hatua. Wakati huohuo, wajumbe wa UEM wameombwa kukusanya vitu mbalimbali kutoka majimbo haya matatu ili vitumike ndani ya jumuia hii ya UEM. Hiki ni kipeperushi, ambacho kimeandaliwa na mchungaji kutoka Ujerumania, mwanamuziki kutoka Indonesia na mwalimu wa muziki kutoka Tanzania. Kusudi lake ni kutumika kama msaada katika kazi mbalimbali zitakazohusu tabia ya nchi na maisha ya kiroho (Climate Spirituality) kama vile ibada, sala, na kutafakari maneno ya Biblia katika sharika ndani ya UEM. Kipeperushi hiki kitakuwa pia katika lugha za Kijerumania, Kingereza, na Kifaransa. Kinaweza kupatikana pia katika mtandao wa UEM ([www.vemission.org/climatespirituality](http://www.vemission.org/climatespirituality)). Wote wenye shauku ya kutoa mchangano wao juu ya uhusiano wa tabia ya nchi na maisha ya kiroho wanakaribishwa na mchangano wao utajumuishwa katika mtandao huu miaka ijayo.

Jochen Motte

# Utangulizi

## Ione dunia kwa macho ya ki-Mungu



*Wahusika wa haki katika hewa: Imelda Simangunsong, Jenitha Kameli, Christian Sandner (kutoka kushoto)*

3

Changamoto za mabadiliko ya hali ya hewa na uharibifu wa mazingira zinaweza kutufanya tujisikie hatuna nguvu na tunaweza kujisikia hatuna msaada wowote. Au tunaweza kulazimishwa tuwe mstari wa mbele (activism) kama wakristo katika kuonyesha tunawezaje kuzuia changamoto hizi kuendelea. Lakini, kama jumuiya ya makanisa, tunaweza kumhusisha Mungu ambaye hutupa nguvu ambayo hutuwezesha kukabiliana na kudhibiti uharibifu huu kwa nguvu ya imani yetu. Mungu kawapa watu wote ardhi kwa ajili ya maisha yao na maji kwa ajili ya afya zao. Katika hewa tunapumua na kwa njia hiyo tunaweza kuhisi uwepo wa roho mtakatifu: ambaye ni pumzi ya maisha ambayo Mungu humpa kila mwanadamu.

Tunajua kwamba, nguvu itokayo kwa Mungu itabubujika tunapoamua kufungua mioyo na akili zetu ili kumruhusu roho mtakatifu wake kuingia. Kwa ajili hiyo, tumeshaweka mkakati ambao lengo lake ni kulifanya suala la haki ya hali ya hewa kuwa sehemu ya ibada zetu kama kanisa. Maswala ya mabadiliko ya hali ya hewa na mazingira yanapaswa kuwa sehemu ya kiroho, kwa sababu ardhi, maji na hewa ni sehemu muhimu katika uumbaji wa Mungu. Tunakuhimiza hata wewe kuona umuhimu wa hali ya hewa katika roho ili nguvu ya Mungu ituongoze tunapofanya sehemu yetu katika kuhifadhi uumbaji wake. Nguvu za Mungu zitatusaidia pia katika mahojiano ili kupambana na nguvu ambazo huharibu msingi wa maisha: serikali, makampuni na mtumiaji mmoja mmoja.

*"Kutambua uwepo wa Mungu, kunatufanya kuwa na mapumziko kutoka katika kufanya kazi zetu za kila siku.. Kutunza siku ya Bwana ni pamoja na kuweka nafasi ya dunia kujirekebisha yenyewe. (65) Liturgia hutusaidia sisi kama wakrito kujifunza taratibu na kuionna dunia kwa macho ya ki-Mungu- yenyeye dira isiyo na mwisho. Misingi hiyo inaweza katuongoza katika jamii kuelewa mitazamo yote ya maisha. (16)" Maneno haya kutoka kwenye utafiti kutoka Afrika ya Kusini juu ya mabadiliko ya hali ya hewa, yametuongoza na kututia moyo katika kushirikishana uzoefu wa kiibada kutoka mataifa mbalimbali.*

Tumekusanya uzoefu kutoka makanisa shiriki ya Afrika, Asia na Ulaya – na tunawashukuru wote waliochangia. Lakini huu ni mwanzo tu. Sehemu ndogo zilizochaguliwa za maombi, rasilimali za liturgia na maneno ya Biblia na mahubiri pamoja na nyimbo kutoka tamaduni tofauti tumezipokea. Ni matumaini yetu kwamba tutaweza kukusanya zaidi ambavyo tutaweza kugawiana wakati wowote tutakapokuwa pamoja na pia kuwekwa katika mtandao wa UEM.

Tunatumaini kwamba baraka za Mungu zitatuimarisha!

*Imelda Simangunsong, Jenitha Kameli, Christian Sandner*

# 1. Ardhi - mama wa maisha

## Wimbo

### Oh Andiko Jilena – Oh jinsi inavyopendeza, Indonesia

Muziki: Ph. Surbakti (1987), Indonesia | Maneno: S. Tarigan (1997), Indonesia

4

**Oh Andiko Jilena**  
*Oh How Beautiful*

GBKP Hymn Book  
Song: Ph. Surbakti, 1987  
Lyrics: S. Tarigan, 1997  
English version:  
Matt Ashworth, Imelda Simangunsong

Karonese, Indonesia

The musical score consists of three staves of music in G clef, common time, and a key signature of one flat. The lyrics are written below each staff, with some words in Indonesian and others in English. The lyrics describe the beauty of nature and the Lord's creation.

Oh an - di - ko ji - le - na, ti - ne - pa Di -  
Oh can you see the beau - ty, of the Lord's cre -  
ba - ta, Su - buk per - ti - bi en - da,  
a - tion. This spec - ial place call'd Ear - th  
ras i - si - na k'ri - ma. De - leng si me -  
and all liv - ing th - ings. There are gre - en  
ra - tah ke - ra - ngen Pe - rik - pe - rik re - nde ka - ba - ngen. An - di - ko ji -  
moun - tains and for - ests where the birds fill the air with their sing - ing. Oh how beau - ti -  
le - na si ban - Na. Seh kel kap u - li - na. E - ma - ka ta - ngar - lah min ki - ta  
ful is the wo - rld that the Lord has giv - en. And that is why we beg man - kind to  
jel - ma, O - la me - la - sang o - la me - tur - dak - sa, Lit te - nah ka - ta pe - dah ni Di -  
he - ar The cries of na - ture liv - ing in fe - ar the Lord has giv - en a mess - age that  
ba - ta. Ja - ga ke - le - ngki, k'ri - na ti - ne - pa - Na.  
is clear and we must love and save ev'ry - thing He has cre - a - ted.

### Oh Andiko Jilena – Oh jinsi inavyopendeza, Indonesia

Oh, je, waweza kuona uzuri wa uumbaji wa Mungu?  
Sehemu hii iitwayo dunia na viumbe vyote viliviyomo.  
Kuna milima na misitu ya kijani na yenye afya nzuri  
Ambapo ndege husikika wakiimba kwa furaha Oh,  
angalia uzuri wa ulimwengu ambao Mungu ametupa

Uzuri huu ndio unatufanya tuuombe ulimwengu kusikia  
Vilio vyta viumbe asilia viishivyo kwa hofu  
Mungu ametupa ujumbe wa uhakika  
Kwamba ni lazima kupenda na kutunza  
Kila kitu ambacho Mungu ameumba

### Oh how beautiful, Indonesia

Oh can you see the beauty of the Lord's creation?  
This special place called Earth and all the living things.  
There are green mountains and forests  
Where birds fill the air with their singing  
Oh how beautiful is the world that the Lord has given

And that is why we beg mankind to hear  
The cries of nature living in fear  
The Lord has given us a message that is clear  
And we must love and save  
Everything He has created

# Maandiko ya Biblia

Mambo ya Walawi 25:19

Nayo nchi itazaa matunda yake, nanyi mtakula na kushiba na kuketi humo salama.

Zaburi 24

5

## Fikara / tafakari

Mambo ya Walawi 25:1–8

Mwaka wa Jubilii uko wazi katika kuwaachia huru watu na mali zao. Pia, mwaka wa jubilii ni kipimo cha bei au uhuru wa kuuza na kununua ardhi na mali nydingine anazozimiliki mtu. Ilionyeshwa katika sheria kwamba ardhi ambayo ni mali ya familia isiuzwe. Sheria iliruhusu mtu kukopesha ardhi kwa muda fulani na kumrudishia mmiliki au warithi wake katika mwaka wa jubilii. Majadiliano ya bei yaliendana na sheria hii: Msidharauliane, wala kuoneana, bali mumwogope Mungu. Na kitu cha mwisho, jubilii ni siku ya watu kurudishiwa mali zao. Kwa hiyo, jubilii ni mwaka wa kupata uhuru, wa kupewa msamaha au adhabu, ni mwaka wa kurudishiwa mali ikiwa ni ardhi na kuachia huru watumwa na kwa namna hii umaskini ungepungua.

Mali na wamiliki wanakuwa pamoja tena. Sheria inawawezesha watu kutunza makabila na familia za watu kwa uhakika, wakati huohuo wakisubiri kurudi kwa Mesia. Kama watu walikua watumwa wanarudishiwa uhuru wao katika mwaka wa jubilii. Hii ilikuwa alama ya wokovu kutoka kwa Kristo ambayo ilithibitisha katika kuwaachia watu huru kutoka katika dhambi na shetani na kuwarudisha tena kuwa watoto huru wa Mungu. Wazo hili la jubilii ni alama inayotukumbusha umiliki wa mali, hasa umiliki wa ardhi kwamba ni haki ya watu wote bila kubagua.

*Askofu Dk Stephen Ismail Munga, Tanzania, Ibada ya Amani Duniani, Medan, Indonesia, 2012*



# 1. Ardhi – mama wa maisha

## Sala

### Wimbo unaohusu Mazingira

6

Mungu, Baba yetu mwenye uuumbaji wa hali ya juu na mwenye nguvu isioelezeka  
Oh, wewe ni muumbaji wa pekee  
Nchi yangu nzuri sana  
Lulu ya bahari ya Hindi  
Ni zawadi ya bure kutoka kwa Mungu  
Oh, Bwana Yesu, tunaomba msaada wako  
Tuweze kuzitunza hazina hizi za thamani  
Za mito, maziwa na mimea inayopendeza  
Uzuri wa nchi ni baraka kwetu  
Tunapaswa kusafisha uchafu uliozagaa katika mazingira yetu  
Kulinda na kutunza wanyama na misitu  
Oh Bwana Yesu tusaidie  
Kutunza urithi huu wa thamani

*Malsha Nawanjani, muumini wa kanisa la Methodist  
Bandarawela, Sri Lanka*





7

## Simulizi

Benzoin historia – Mahusiano mabaya ya Toba  
Pulp Lestari (TPL), Indonesia

## Sala

Sala ya kuomba msamaha

Unaweza kuendesha kwa muda wa masaa mawili kutoka katika kiwanda cha karatasi, ukiwa katika msitu mzito. Kama baba na babu yake, Hapusan Sinembela huishi akitegemea resin inayotokana na miti ya benzoin. Katika aina hii ya miti, Hapusan hutengeneza manukato. Miti hii imezagaa katika vichaka na hutunzwa kwa nyimbo zinazoimbwa mara kwa mara. "Oh, binti yangu, Baba yako amepumzika sasa. Oh mpendwa binti kua vizuri..." Lakini miti yangu ipo hatarini maana mashine zinazoharibu misitu zimeharibu kukua kwake. Misitu ya benzoin ambayo wenyiji wanaienzi mashine imezikata na mikalitisi imepandwa na wamiliki wa viwanda vya kutengeneza karatasi. Udongo mzuri wa misitu umevamiwa na mwisho wake utakuwa haufai tena maana utakuwa umeharibiwa.

Maisha ya watu, vizazi na vizazi yalikuwa yakitegemea miti ya benzoin. Unapoangalia miti hii, inaonekana kana kwamba ni miti ya asilia lakini imepandwa. Miti hii huangaliwa kwa makini na kutunzwa na watu vizuri sana kana kwamba ni watoto. Kwa sababu ya faida wanayoipata, miti hii hupendwa sana na hutunzwa kwa uangalifu wa hali ya juu. Wanyama wengi huishi ndani ya misitu hii. "Iwapo tutakata tamaa na kuacha kupigania ardhi yetu tukaiachia Toba Pulp Lestari, watu watakuwa watumwa wa makampuni yanaotumia misitu hii kwa ajili ya kutengeneza karatasi. Na hilo nitatukosesha amani kabisa".

Mungu Baba, tunajua kwamba wewe ni muumbaji. Ulituumba kwa mfano wako. Ulitupa jukumu la kutawala dunia na vilivyomo vyote. Tunatubu kwamba hatujawa watunzaji wazuri wa uumbaji wako. Tumesababisha ongezeko la joto duniani kwa kutokana na kuchoma mafuta na gesi. Tumekata miti mingi bila kupanda mingine, tunatumia teknolojia za mashine na kuharibu hali ya hewa, tumepata faida kubwa kutokana na maliasili mbalimbali lakini hatujawalipa wamiliki wa ardhi sawasawa kutokana na faida hiyo. Mwenyezi Mungu tupe busara zako ili tuweze kukumbuka kutunza mazingira yetu. Tusaidie ili kila wakati tuwe tukikumbuka jinsi ya kutumia vizuri maliasili zetu ili tusiwe tunaziharibu kwa ajili ya kupata faida. Tunaomba vyote hivi kapitia kwa jina la Bwana wetu Yesu Kristo. Amina.

Mch. Emmanuel Ngambeki, Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania, Dayosisi ya Karagwe (ELCT/KAD), Tanzania

*Imetokana na filamu, "A light for every hut" iliyotengenezwa na Johannes Meier, Ujerumani*

# 2. Maji - Chimbuko la Maisha Wimbo

Tusisahau Kutunza Mazingira – Rwanda – Let's remember, Rwanda

Muziki na Maneno: Poul Bayona | English: Philipp Sandner, Germany

**Tusisahau Kutunza Mazinga - Let's remember**

Ndu-gu za-ngu tu - si - je tu - ka - sa - ha - u ka - zi  
Let' re - mem-ber, my sis-ters, bro-thers, re - mem-ber: our -

ye - tu mu hi - mu ya ma-zí - gi - ra mwa - ya - o - na -  
na - ture we have been giv-en to care for. When for years we

ya - me - a - nza ku ha - ri - bi - ka mu da ndi o hu - u ku -  
have - done our best to de - stroy it - take re - spon-sa - bi - li - ty.

*Refrain*

a - za wa - ji bi - ka Tu - a - mu - e mo - ja  
Time is now for ac-tion. Let us speak with one voice

kwa-mba tu - ya - li nde ma-zí - ngl - ra ye - tu kwa ma - nu -  
and try to pre-serve it. It's in our own in - terest to pre-serve

fa a ya - tu.  
our en - vi - ron - ment.

## Mapendekero

**Mungu, miungu na Ukame**

Wakati akijadiliana na Ahabu, mfalme wa Israeli, nabii Eliya katangaza ukame mkubwa sana ambao ungelikumba dunia kwa miaka mungi. "Hakutakuwa na umande wala mvua miaka hii" (1 Wafalme 17:1). Ahabu alikuwa ameanzisha ibada ya Mungu wa mvua Baali katika Israel (18:18). Lakini watu wa Baali hawakubadilika. Matokeo yake, mvua iliacha kunyesha na njaa kubwa ikatokea katika Samaria (18:2).

Ukame na njaa ni majanga ya siku hizi. Katika nchi za Somalia, Ethiopia, Kenya – ukame na njaa ni majanga yaliyotakana na mabadiliko ya hali ya hewa. Wakati wa Elijah na Ahab, njaa na ukame havikusababishwa na

mabadiliko ya hali ya hewa bali ni kutolewana kati ya watu na miungu yao. Uamuzi ulipaswa kutolewa: ilipaswa kujulikana kwamba waisrael wanamfuata nani, wanamsujudu nani na wanamwamini nani? Swali lilikuwa: Waliamini nini kilichosababisha uharibifu huo? Kama kielelezo kwetu, Swali kwetu linakuwa: tuna imani ipi nyakati hizi inayosababisha kuwepo kwa mabadiliko ya hali ya hewa? Tunamwamini nani ambaye anasababisha majanga?

Tumeweza kuelewa nguvu zinazojaribu kutudhibiti na tukiri kwamba mara nyingine nguvu hizi hufanikiwa. Kitu kimojawapo ni "kukua kwa uchumi". Inafahamika kwamba

kuzalisha kwa faida kumetokea baada ya maendeleo ya mwanadamu na hitaji hilo limeweza kufanikiwa kwa kiasi kikubwa. Sambamba hayo, hata hivyo, neno "kukua kwa uchumi" – ni aina ya kiinimacho. Siasa na uchumi inaona kukua kwa uchumi kama dawa na tegemeo linaloweza kutatua shida za siku hizi. Lakini wakati huohuo, wingi wa ukuaji, unasababisha uharibifu zaidi na mpya unaopelekaa kuharibika kwa uchumi na uasilia wa ekolojia. Hivi ndivyo wasioelewa (wanaofananishwa na miungu) walivyo: wanaahidi maisha ambayo yanatupeleka katika kifo.

"Kuhama" ni nguvu nyingine. Zaidi ya miaka mingi, watu wamevumbua uwezekano wa kuhama kutoka sehemu moja kwenda nyingine kwa uhuru duniani. Lakini

mafanikio haya yamesababisha mtu kutegemea kitu kingine ili aishi, yameleta sheria zake na zinaleta wasiwasi kwa watu na zinaharibu mazingira. Hivi ndivyo nguvu za wasiojua zinavyofanya, wanaahidi uhuru unaopeleka watu kuishi kwa kutegemea vitu vingine. Kwa kawaida sio rahisi kujibu swali hili: ni lini kukua kwa uchumi na kuhama kutaimarisha maisha ya watu na ni lini nguvu zinazojitegemea zitabadilika na mwisho wapende kutoharibu utu?

*Rev. Dr Eberhard Loeschke, Kanisa la Kiinjili la Rhineland (EKiR), Germany*



## Simulizi

### Zawadi za Mungu ziko Hatarini


Hatuwezi tu kukaa na kuangalia jinsi dunia inavyoharibika kutokana na shughuli za binadamu. Mabadiliko ya hali ya hewa sio utani na kila mwanadamu anapaswa kujumuika katika kuzuia uharibifu kabla hatujachelewa. Pamoja na ishara nyingi zinazotishia uasili wa dunia ambazo zinaweza kuathiri sana maisha yetu, nimeshuhudia katika namna ndogo lakini ya kuhuzunisha kwamba hata UPEPO unaweza kuwepo kwa nadra. Zamani, sikuwanafikiri sana kwa makini juu ya umuhimu wa upепо katika maisha yetu, mpaka ilipofika mwezi wa Desemba 2011 na Januari 2012. Upепо unaweza kuwa tatizo katika sehemu fulani fulani za nchi yetu na kuna sehemu nyingine ambapo upепо ni mwangi zaidi. Lakini hata kama upепо unaweza kusababisha maafa, ukosefu wa upепо unaweza kusababisha masononeko makubwa sana na sio kwa wanadamu peke yake lakini hata kwa wanyama wanaofugwa .

Nilipokuwa nikitatufuta mahali pa kupumzikia baada ya kazi nyingi za mwaka, nilifanikiwa kwenda kupumzika kwa siku chahe katika nyumba ya wakulima. Kama tunavyoju, maji ni muhimu sana katika maisha ya mwanadamu na kwa wakulima katika nchi ya Namibia, kuna mashine zinazotumia upепо kwa ajili ya kutoa maji ardhini. Kwa siku kama tatu mashine hii haukuweza kuzunguka kabisa. Ilionekana kana kwamba kila kitu kilichokuwa kimekuwa hata tone la maji halikuonekana na wala hapakuwepo na alama ya maisha. Joto lilikuwa jingi sana kiasi kwamba ilikuwa vigumu kulimudu. Ingawa hatukuweza kupima kwa kutumia kipima joto, ni lazima ilikuwa kama nyuzi-joto zaidi ya 45. Wanyama hawakuweza kumudu ukali wa joto, walikuwa akitafutatafuta vivuli ndani ya shamba

walimokuwa wakiishi. Pamoja na hali mbaya ya kutovumilika, mashine ya upепо ya kuleta maji haikuonyesha dalili ya kuzunguka kwa sababu upепо haukuwepo. Huu ni uvumbuzi wa kushangaza: kwamba hata upепо unaweza kukosekana kwa sababu ya mabadiliko ya hali ya hewa!.

Hii ilinifanya nitambue, kwamba wito kwa watu wote dunia nzima kwamba tunapaswa kujumuika katika kuitunza dunia, ni wito ambao kila mmoja anapaswa kuuchukua kwa makini sana. Serikali zetu, makanisa yote na makampuni yote yanapaswa kuangalia umuhimu wa kutunza dunia hii kwa kuandaa mikakati. Mungu kwa mapenzi yake aliweka wakati wa kupanda na wakati wa kuvuna, wakati wa mvua na wakati wa kiangazi na vyote vinavyotusaidia katika maisha, lakini vyote viko hatarini, na maskini wa chini kabisa ndio watakaoathirika zaidi. Mungu aliumba nchi inayotoa matunda kwa ajili ya mahitaji ya watu lakini kila kitu kimeharibiwa kwa sababu ya ubinafsni na tamai. Mungu alitupa uhuru wa kutawala dunia na vilivyomo na kwa sababu hiyo akatufanya kuwa watunzaji pamoja naye wa uumbaji wake. Tumuombe Mungu atupe hekima, akili na utayari wa kutumia rasilimali ili asiwepo ye yote atakayeumia kwa sababu ya matumizi mabaya ya rasilimali hizi na hii itavifanya vizazi vijavyo vimsifu Mungu kwa uzuri wa uumbaji wake. Mungu awawezeshe wale wote wanaofanya kazi ya kutunza dunia kwa ajili ya maisha yajayo.

*Rev. Hatani Kisting, Makamo wa Raisi Kanisa na Kiinjili la Kilutheri Namibia (ELCRN), Namibia*




## 2. Maji - Chimbuko la Maisha

# Maneno ya Biblia

Mwanzo 9

Zaburi 1:3



10

## Simulizi

### Uzoefu kutoka Uphilipino

Walipokuwa usingizini usiku wa manane tarehe 16 mwezi wa 12 mwaka 2011, maelfu ya watu walishitushwa na upepo mkali unaojulikana kama "Sendong" na maji mengi yaliyosababisha mafuriko na kubomoa nyumba zao na miundo mbinu ya maendeleo yao. Zaidi ya watu 1,453 walikufa. Maji haya ya ghafla yalitoka milimani na yalisababishwa na mvua kubwa iliyonyesha kwa masaa 12 ambayo ilijaza sana mito na kusababisha mafuriko. Mvua hii ilikuwa kubwa sana na ilikuwa mara ya kwanza kunyesha katika sehemu hii ya kaskazini mashariki ya Mindanao, katika nchi ya Philippino. Mvua hiyo imesababishwa na uharibifu wa mazingira.

Hali kama hii ilitokea tena tarehe 9 mwezi wa 8 mwaka 2012, katika miji kumi ya manispaa katika sehemu za Metro Manila na majimbo 6 eneo la Luzon. Katika sehemu hizi, mafuriko yalisababishwa na mvua kubwa ilionyesha siku kadhaa.

Maafa haya yaliyotokea miezi michache iliopita, yanaonyesha jinsi uumbaji wa Mungu unavyoharibiwa na majira ya nchi. Hali yetu ya mazingira imebadilika sana. Mzunguko mzuri wa majira ya mvua na kianganzi umevirugwa. Hatuna tena hewa nzuri ya kuvuta na maji ya mito na maziwa si masafi na hayatiririki ipasavyo. Hatuwezi tena kukaa juani hata saa moja asubuhi kwa sababu juu ni kali sana hata wakati wa asubuhi.

Kanisa la Muungano wa Makanisa ya Kikristo la UPhilippino (UCCP), ambalo ni kati ya makanisa 34 ya United Evangelical Mission (UEM), linaamini kwamba, wanadamu wamepewa jukumu la kutunza na kutetea kila kitu ambacho Mungu ametengeneza ikiwemo ardhi, bahari, hewa, maji, ndege, mimea na viumbe vyote viishivyo. Mungu aliwaumba wanadamu kuwa wasimamizi wa

uumbaji wake. Lakini wanadamu wameshindwa sana kutimiza jukumu hili.

Kwa kuwa mwanadamu amekuwa na hamu ya kumiliki mali nyingi hapa duniani, pamoja na matumizi mabaya ya ardhi bila kujali ustawi wa uumbaji wa Mungu, wanadanmu, kwa mfano, wamejikita katika uchimbaji wa madini na kuwa na viwanda vingi, ambavyo vimesababisha maafa makubwa sehemu mbalimbali hapa duniani. Vitendo hivi vimesababisha kuisha kwa misitu na kuharibika kwa milima. Cha kusikitisha zaidi i, mvua zinaponyesha, mito inashindwa kuhimili maji maana milima imeharibiwa. Hivi vimesababisha kutoweka kwa misitu kwa haraka pamoja na milima. Mvua zinaponyesha mito inafurika na mafuriko hutoke na kuharibu miji na mashamba.

Maridhiano kati ya uchumi na uasilia wa mazingira unahitajika haraka ili kupunguza ongezeko la maafa ya mambo ya msingi ya mwanadamu duniani kote. Sio wale wanaojaribu kutunza mazingira waonekane kama "maharamia" hapa bali wale ambao wanaharibu mazingira kwa ajili ya "faida" na "uchoyo wa pesa"

Nahisi kwamba, Uphilippino sio nchi pekee ambayo imeishapata maafa kama haya yanayo sababishwa na mabadiliko ya hali ya hewa. Kwa hiyo, ni changamoto ya kila mmoja wetu ajisikie anahusika katika utunzaji wa uumbaji wa Mungu. Mungu alitufundisha kuitunza dunia, na kama tukitimiza jukumu hili, hali ya hewa na mazingira vitaendelea kufurahisha vizazi baada vijavyo.

Elsie Joy Dela Cruz, Pastor, Umoja wa Makanisa ya Kikristo Philippines, Philippines





# Sala

## Wito wa Kuabudu

Ni lazima tumuombe Mungu atusaidie  
Mungu alipoumba mbingu na dunia  
aliweka mipaka na kikomo  
Na aliona inafaa  
Lakini miaka hii, joto linaongezeka na theluji inayeyuka.  
Kwa sababu hii, mito na bahari vinajaa na kujaza sehemu  
ya ardhi ilio kavu.

Wanasema Mungu aliumba mbingu na dunia  
Mungu akayatenga maji sehemu yake na pakavu sehemu  
yake.  
Lakini sasa jangwa linaongezeka na watu wameanza  
kutawanyika na kuwa wakimbizi wakitafuta mahali  
panapofaa ili wajihifadhi.

Ni lazima tupambane kwa nguvu zetu zote ili tuzuie  
mabadiliko ya hali ya hewa,  
Tufanye kazi hii pamoja ili tuokoe uumbaji wa Mungu  
ambao hata sisi ni sehemu yake.  
Ni lazima tuombe msaada kwa Mungu .

*Keld B. Hansen, European Christian Environmental Network  
(ECEN), 2009*

## Mchezo – Maji – Uhai – Kifo Mungu muumbaji mwenye upendo

- K** Mungu muumbaji mwenye upendo,  
Unajali Ardhi kwa kuinyeshea mvua;  
Unauezesha udongo kuwa na rutuba na kutoa  
matunda.  
Na kweli inauwezesha udongo kutoa mazao ya  
kutosha!
- W** Vyote vilivyoumba vinaimba kwa furahai.
- K** Tutakapo itunza Ardhi,  
Tutapanda na kuvuna,  
**A** Viumbe vyote vitaimba kwa furaha.
- L** Tutakapo tunza mito mikubwa na midogo,  
Tutakapothamini uasili wa maziwa na bahari,  
**A** Viumbe vyako vitaimba kwa furaha.
- L** Tutakapopambanua kwamba watu wote ni  
familia moja,  
Kaka na dada wanaojumuika,  
katika kutunza Ardhi na maji,  
**A** Viumbe vyote vitaimba kwa furaha  
kwani unavibariki kwa wingi siku zetu zote.

*Per Harling, from Gloria Deo, Sala na nyimbo kwa ajili ya e  
Mkutano Mkubwa wa 12 wa Makanisa ya Ulaya (CEC), 2003*



# 3. Hewa – Punzi ya uhai

## Wimbo

Disabar! – Kuwa mwerevu na mvumilivu!, Indonesia

12

**Disabar!**  
*Be Patient!*

Javanese Language, Indonesia

Song & Lyrics:  
Sutarto (GKJTU, Indonesia)

The musical score consists of three staves of music in G clef, 2/4 time, and a key signature of one flat. The first staff starts with a rest followed by a dotted quarter note. The lyrics are: "Di - sa - bar, o - jo gam-pang ne - su! Di - sa - Be pa -". The second staff begins with a dotted quarter note. The lyrics are: "bar, o - jo gru - sa - gru - su! Di - sa - bar, o - jo ngge - ge-mong-". The third staff begins with a dotted quarter note. The lyrics are: "tient don't a - ct has - til - ly Do not run be - fore you can". The fourth staff begins with a dotted quarter note. The lyrics are: "so! Gus - ti - a - sih wong sa - bar pra - ca - ya. walk The Lord loves those who are ke - en and be - lieve." The fifth staff begins with a dotted quarter note.

## Maneno katika Biblia

Zaburi 104:30

Utumapo roho wako, vinaumbwa;  
na unatengeneza kwa upya sura ya udongo.  
Kumbukumbu la Torati 20,19:20



## Kudhibitisha


### Jukumu juu ya Uumbaji wa Mungu

Katika imani ya Kikristo, kila mmoja ana namna mbili. Kwa namna moja, tu viumbe kati ya viumbe vingine. Lakini pia kwa namna nyingine, tumeumbwa kwa mfano wa Mungu. Kama wanadamu, tunaweza kudhibitisha sisi ni wa namna gani na tukoje kwa matokeo ya mambo tunayoyafanya. Kwa hiyo, tunabeba jukumu tofauti na viumbe wengine katika kutunza uasilia wa uumbaji wa Mungu kwa kulima na kutunza dunia kwa uaminifu.

Sio kwamba kupewa mamlaka yasio na kikomo kuitawala dunia kutoka kwa Mungu na uwezo wetu kuitiisha dunia vitufanye wanadamu tuwe na "kiburi cha kuumbwa". Hatutakuwa wanadamu walioumbwa kwa mfano wa Mungu kama hatutafanya jukumu letu la "kutunza" uumbaji wa Mungu.

Sheria inayoongoza Sabato na maeleo yake vinaonyesha "kulima na kutunza" uumbaji wa Mungu. Sheria hizi msingi wake ni kusimamia kanuni kwamba pasiwepo na vikwazo na matumizi mabaya ya udongo, wanyama, na wanadamu. Zinasimamia katika kupinga kutokuwa na mipaka na ubadhilifu. Pia tunapaswa kuwa na sheria kwa ajili yetu wenyewe na kuzifuata. Kuhusiana na mabadiliko ya hali ya hewa, hii mipaka ina maana ya kwanza, kupunguza kabisa kemikali zinazosababisha uharibifu wa hali ya hewa na kukataa kabisa kuongezeka kwa viwanda kama vile vinavyopatikana katika nchi kama Ujeruman. Kuongezeka kwa viwanda kunasababisha kuharibika kwa uasilia wa nchi na watu wake. Na mipaka mingine ni katika kugawana kwa uwiano rasilimali tulizopewa na Mungu ili kufanya maisha yawe rahisi kwa wanadamu na wanyama.

*Katja Breyer, Kanisa na Kiinjili la Westfalia (EKvW),  
Ujerumani*



### 3. Hewa – Punzi ya uhai

## Simulizi

### Bei ya oksijeni na mikakati ya upandaji miti.

14

Siku hizi katika mitando, kuna habari zinazohusu bei ya oksijeni na umuhimu wa miti. Habari hizi zinasema, "Kwa siku moja, mwanadamu anavuta oksijeni kiasi cha silinda 3. Katika kila silinda ya oksijeni, bei yake ni rupia (Rs pesa ya India). 700/- Kwa hiyo, kila siku, kila mwanadamu hutumia oksijeni kwa bei ya rupia. 2,100/- na kwa mwaka mzima mtu mmoja hutumia rupia 766,500/- bila riba. Tukiweka kiasi hiki cha fedha katika muda wa kawaida wa mwanadamu kuishi, kwa mfano miaka 65, kila mtu anatumia oksijeni inayogharimu kiasi cha rupia 50,000,000/. Ukibadilisha pesa hii kwa pesa ya ulaya zinakuwa 700.000 ambazo ni shilingi 1,400,000,000/ (shilingi ya Tanzania). Kiasi hiki cha oksijeni kinatumika bure kutokana na miti na mimea mingine iliyotuzunguka. Hata hivyo ni watu wachache sana wanaothamini kuwepo kwa miti. Kwa sababu hii, watu walio wengi hukata miti ovyo bila kujali. Ni lazima vitendo vya ukataji miti viachwe mara moja.

Mwishoni, kila mmoja anaombwa kutuma ujumbe kwa rafiki zake ili nao pia wajumuike katika utunzaji wa miti na mimea ili tuendelee kupata oksijeni ya bure.

Hii ni hadithi tu na bei yenyewe ya kununua oksijeni haiwezekani. Hata hivyo, inatia uchu na inaonyesha

umuhimu wa kuwepo kwa miti katika maisha yetu. Katika dunia hii, tunaona watu walivyo na hamu ya kutengeneza misitu, wakati huohuo watu wengine huharibu misitu. Miti na misitu hufyonza hewa chafu iliopo angani na pia huwezesha upatikanaji wa oksijeni. Kwa nchi zinazoendelea, hasa Afrika, miti ni muhumu sana kwa sababu ni chanzo cha nishati. Utumiaji wa kuni ni asilimia 90 ya jumla ya nishati zote katika nchi hizi. Hizi ndizo sababu kubwa zinazosababisha ubadhilifu wa mazingira kwa sababu ya uharibifu wa misitu.

Kwa hiyo, kuna uhamasishaji wa matumizi mazuri ya nishati kwa kutumia majiko yasiyotumia mkaa mwingu, kupunguza utumiaji wa miti na uharibifu wa misitu na uhusiano kati ya maisha ya wanyama na dunia. Upandaji wa miti unazuia mmomonyoko wa udongo na upotevu wa virutubisho vya udongo. Kwa njia ya kupanda miti, wakulima wataendelea kupata mazao mazuri na kwa namna hii watu watapata chakula cha kutosha. Kwa hiyo, ni jukumu la kila mmoja kupata na elimu ya kupanda miti katika mashule na vijijini.

*Richard Madete, regional consultant (Africa), UEM climate protection programme, Tanzania*






# Sala

## Kirie

- K** Tumeharibu maisha ya wanyama kwa kuchoma misitu.  
Badala ya kuwa na hewa safi tunakuwa na moshi  
Tunweka sumu katika maji masafi na kuogesha watoto maji machafu  
Tunawaua wajukuu kwa urithi wenye sumu  
Bwana uturehemu.
- W** Kirie, kirie, eleison. Kirie, kirie eleison
- K** Eh Mungu, tunajifanya hatujui maafa ya asili, ila asili ni wewe.  
Hatuna la kusema, tunaogopa sheria zinazoruhusu watu kuharibu uasilia wa dunia. Na tunakuogopa.  
Hata kanisa ambalo ni mwili wako wakati mwingi linanyamaza na kutafuta mahali pengine penye usalama. Eh Mungu, tunasubiri mbingu na dunia zilizo mpya ambapo kweli na haki itapatikana kwa ajili ya uumbaji wako.  
Eh Bwana Utirehemu.

**Wote** Kirie, kirie, eleison. Kirie, kirie eleison.

*Karo Batak Kanisa la Kiporotestantch (GBKP), Ibada ya kufunga, Medan, Indonesia, 2012*



# 4. Nguru – Nguru za Maisha

## Wimbo

Mungu anatoa wito leo – Kutoka Ufilipino

Muziki na maneno: Luna L. Dingayan, Philippines | Ufafanuzi: Perla P. Dingayan, Philippines

16

### God's Call For Today

Words & Music:  
Luna L. Dingayan, 1989  
Transc. Perla P. Dingayan, 1989

The musical score consists of five staves of music in common time, featuring a treble clef and a key signature of one sharp (F#). The score includes lyrics in English and Chichewa. Chords indicated above the staff include D<sup>c</sup>, A<sup>j</sup>, D<sup>c</sup>, A<sup>j</sup>, D<sup>c</sup>, G<sup>c</sup>, C<sup>j</sup>, F, D<sup>c</sup>, B<sup>-</sup>, G<sup>c</sup>, A<sup>j</sup>, A<sup>j</sup>, D<sup>c</sup>, G<sup>c</sup>, B<sup>-</sup>, D<sup>c</sup>, G<sup>c</sup>, F, D<sup>c</sup>, A<sup>j</sup>, G<sup>c</sup>, C<sup>j</sup>, F, D<sup>c</sup>, B<sup>-</sup>, D<sup>c</sup>, G<sup>c</sup>, A<sup>j</sup>, and D<sup>c</sup>. The lyrics describe the call of God to all nations, sharing what we have, and working for justice and restoration.

1 From ma - ny na - tions we have come with  
2 We've heard the les - sons of the past, how  
3 Cre - a - tion groans now in tra - vail, in

4 bur - ning hearts and minds To share to all what we have  
greed des-stroyed hu-ma - ni - ty. The na - tions rise and fall in  
need need of care and dig - ni - ty. Come peo - ple of the world, let's

7 seen and heard as God's call in our lands and seas; We have  
flames of war and the peo - ple live in mi - se - ry.  
share our live for to live is to care for the earth.

10 seen the strug - gles of the poor, we have seen our bond of u - ni -

13 ty we have heard God call - ing us to - day: Pray for

16 peace, work for jus - tice and res - tore cre - a - tion's dig - ni - ty.

## Quotations

"Tulifanya JPIC semina katika sehemu ya Kaliki lakini tulihisi tulikuwa tumechelewa tayari. Makampuni mengi yalishaingia Merauke na pesa imeishaonekana ya muhimu sana kuliko kitu kingine kwa watu." *Dora Balubun, mlatibu wa Haki Amani na umbaji mzima Dawati la Kanisa la Kinjili la Kikristo katika Tanah Sinodi ya Papua (GKI-TP), Indonesia.*

"Kampuni sio mkombozi. Inasema haki ya umiliki wa Ardhi kwa njia ya udanganyifu." *Nicolaus Adi Saputra, Askofu wa Kanisa la Katoliki la Dayosisi ya Merauke, Papua ya Magharibi, Indonesia*

## Makumbusho

### Mungu – Nguvu ya Maisha

Nguvu! Nguvu ni nzuri. Hii ni kwa sababu kila mmoja anapenda kuwa nazo kwa namna fulani – katika familia, kazini, katika siasa, nk. Ndiyo maana ni muhimu kuwawezesha watu kuwa na nguvu kwa namna tofauti tofauti. Lakini nakumbuka sentensi moja inayotokana na filamu ya Spiderman, mzee mmoja alimwambia Spiderman: "penye nguvu nyingi, majukumu makubwa hutokea."

Zaidi ya miaka 100 iliopita, idadi ya watu duniani imeongezeka kutoka watu bilioni mbili hadi bilioni saba. Haishangazi kuona misukosuko ya mazingira ni mikali kwa sababu watu wanapigania kunufaika na vitu asilia ambavyo haviongezeki. Hakuna sehemu ambayo mabadiliko ya hali ya hewa hayajatokea. Wanadamu wamepewa nguvu kubwa ya »kuitawala dunia«, pia tumepewa jukumu kubwa la kuitunza dunia, ni kubwa na ni lazima kulichukulia kwa nguvu zote. Shida ambayo imejitokeza ni kwamba, badala ya kutunza dunia kwa umakini mkubwa, tunafikiria kuitumia bila kuwa makini kwa sababu tu tuna nguvu. Na kati yetu, wale wenye nguvu za siasa na uchumi, wanatumia nguvu hizi kuwagandamiza wengine.

Shida kubwa ambayo ulimwengu haujagundua ni kujuu na kuelewa kusudi la Mungu juu ya uasili wa uumbaji wake katika maisha yetu. Kama tunavyofikiri kwamba tunauwezo juu ya maisha yetu, tunasahau kwamba sisi pia ni watunzaji wa dunia hii. Watu wengi wameacha kumuhusisha Mungu katika shughuli zao kwa mfano kupata kazi mpya, kwenda kuwindia, kuandaa mahala pa ujenzi wa nyumba au maandalizi ya shamba. Watu wengi hawakumbuki hata kumshukuru Mungu wanapopona kutohama na ugonjwa au mtoto anapozaliwa au mtu anapopanda cheo. Mungu hawamjali hata kidogo. Tunafikiria kwamba sisi kama wanadamu tumepata vitu tulivyonyavyo kwa uwezo wetu wenyewe. Tumejichukulia tulivyopewa na Mungu kana kwamba hatukupewa jukumu la kuvitunza. Tunafikiria kwamba dunia ni yetu, lakini kwa hakika, "Dunia na vyote vilivymo ni mali ya Mungu" (Ps. 24:1). Billy Graham siku moja alisema, uvumbuzi wa sayari ya dunia ulimpa sababu ya kumsujidia Mungu kwa sababu Mungu ni muumbaji wa vyote.

Nguvu za Mungu ni za ajabu pia. Tunajiuliza wenyewe mara nyingi, Mungu yuko wapi? Kwanini yuko kimya tunapohitaji msaada wake? Mungu anakuwa wapi ukame unapotokea, upopo mkali, tetemeko, vinavyosababisha vifo vya watu wasio na hatia? Mungu anakuwa wapi maskini

Kutoka 32:1–19  
Zaburi 96:11–13

wanapomuomba wapate msaada wake lakini hajibu lolote wakati walioko katika uongozi selikalini wanaponyanganywa Ardhi yao na kupewa wachimbaji wa madini, watengenezaji mafuta au wawekezaji mbalimbali? Kwanini Mungu hajibu maombi ya waombaji katika kanisa huku watu wanaomba kwa bidii? Maswali kama haya yamekuwa yakinoteka kutoka kwa waumini mara nyingi kutoka vizazi vyote. Na hatuna majibu yoyote.

Lakini tunaelewe jambo hili, Mungu alichagua kufanyakazi na watu duniani. Mungu alitupa jukumu la kulindana na kutunzana sisi kwa sisi. Na mungu alichagua asitupe adhabu kila tunapokosa. Lakini Mungu mwenyewe anatuita kumgeukia na kuwapenda jirani zetu. Mungu hutumia uwezo wake kwa makini. Mungu hamdhuru yejote mwenye dhambi bali humuelekeza ili atubu. Tunaitwa kumgeukia Mungu kwa upendo na kwa njia hii kuihudumia dunia tukiwa na upendo huohuo. Kama hatufanyi hivyo, Mungu anaumia sana kwa uumbaji wake. Mungu ni Mungu ambaye hutumia uwezo wake kwa makini, sio kuwaharibu wasiofanya jinsi apendavyo bali kuwaokoa.

Tutumie uwezo ambaa tumepewa na Mungu juu ya dunia kama vile Mungu anavyotujali sisi. Kutunza uumbaji wake wote kwa upendo kama huu, iwe lengo letu.

*Rev. Dr Fidon Mwombeki, Katibu Mkuu, Misioni ya Umoja wa Makanisa ya Kiinjili*



# 4. Nguru – Nguru za Maisha

## Wimbo

Wandle das Leben – Badilisha maisha yetu, Kijerumani

### Wandle das Leben

Kyrie-Lied zur Kampagne „Klimawandel – Lebenswandel“

2. Es atmet dich, Gott, ein Wal im Meer – Dort lebt er.  
Zieht alleine seine Bahn, ruft stumm sich an – Eleison.
3. Es atmet dich, Gott, eine Eiche im Wald – Dort lebt sie.  
Sie steht traurig da, dem Ende nah – Eleison.
4. Es atmet dich, Gott, ein Adler im Wind – Dort lebt er.  
Schwebt einsam hinan, schreit still dich an – Eleison.
5. Es atmet dich, Christus, die Kleine im Tuch – Noch lebt sie. Sie liegt hungrig da, dem Weinen nah – Eleison.
6. Dein Odem, heilig, durchwehe uns hier – So leben wir.  
Erfrische die Seele, Herz, Mut und Sinn – Eleison.

© tvd-verlag  
Music and lyrics: Mechthild Werner, Till Werner,  
Ujerumani | Satz: Fritz Baltruweit 2010  
English: Christian Sandner

1. Pumzi yako iliyo takatifu imiminike duniani na katika viumbe vyako, irekebishe miyo, roho na mawazo yetu. Eleison

Chorasi:

Badilisha maisha yetu, badilisha mawazo yetu,  
badilisha ulimwengu:  
Ninapumua, Mimi. Badilisha maisha yetu, badilisha  
Maisha yetu, badilisha ulimwengu: mimina pumzi yako  
katika ulimwengu ili ubadilike.

2. Pumzi yako, Eh Mungu,  
mimina kwa samaki wa baharini na wanyama wote.  
Eleison.
3. Pumzi yako, Eh Mungu, imiminike katika miti na  
viishivyo.  
Inahuzunisha kwamba mwisho wake u-karibu: Eleison.
4. Pumzi yako, Eh Mungu, ipae angani kwa viishivyo:  
Eleison.
5. Pumzi yako, Eh Kristo, katika mtoto mdogo, aishi.  
Kitoto kimelala na njaa na kinalia kwa sauti ya unyonge:  
Eleison.
6. Pumzi yako takatifu, Mungu, iachie itumiminikie,  
kwa ajili ya maisha yetu.  
Rekebisha miyo yetu, na roho zetu na akili zetu: Eleison.

# Simulizi

## Na mwekezaji aleta mwanga

Siku chache zilizopita Matius alipata simu ya mkononi – na alikuwa na dhamira mbaya. Pamoja na viongozi wengine wanne wa kimila wa Papua, Matius aliwekeana mkataba wa sehemu kubwa ya ardhi ya kijiji hicho na kiwanda cha sukari kiitwacho Rajawali sugar-cane company. Au labda ameuza, hakuna mwenye uhakika. Mwishoni, siku moja katika mwezi wa tatu, wakati usiku unaingia, waliwazunguka na kuwalazimisha wanakijiji watoke katika ardhi ile.

Uporaji wa ardhi una sura nyingi. Katika nchi ya Indonesia, kama ilivyo katika nchi nyingine barani Asia, vijiji vingi vimehamishwa na kuwekwa sehemu nyingine ili kupisha wawekezaji wa ndani na nje.

Jambo la kuwa na hati ya ardhi limeishagombaniwa katika nchi ya Indonesia. Kufuatana na sheria ya nchi, ardhi ni mali ya serikali – isipokuwa kama mtu atadhibitisha kwamba ni mmiliki halisi wa ardhi fulani. Lakini jambo la kuwa na hati halijawahi kutokea kwa sababu hati za namna hiyo zilikuwa hazijawahi kutolewa kwa wananchi siku za nyuma. Kwa sasa bado serikali haitaki kutoa kibali cha mtu kuwa na hati miliki ya ardhi yake kama ilivyokuwa hapo awali. Kwa namna hii, serikali inakuwa na uhuru kumilikisha ardhi kwa wawekezaji wenyewe pesa nyingi. Uamuzi huu ni kinyume na azimio la umoja wa mataifa unaohimiza kujali maslahi ya wananchi ambayo humaanisha kwamba kabla ardhi hajauzwa kwa wawekezaji, ni lazima watu waridhie ndipo ardhi iuzwe. Lakini serikali ya Indonesia haitambui

kwamba Indonesia ni mali ya waindonesia. Lakini kama sheria za mitaa na mikoa ni adilifu na zinafuata mafundisho ya Jakarta, wawekezaji wanamaliza kwa kuongeza mikataba zaidi na wananchi katika mitaa yao.

Kijiji cha Matius ni mwanzo tu. Kristina Neubauer, mratibu wa West Papua Network (WPN) na Faith-Based Network katika Papua ya magharibi (FBN), alifanya majumuisho kwamba katika miaka 10 ijayo, Papua itaonekana kama Sumatra ya kaskazini inavyoonekana kwa sasa. Ilikuwa mwezi wa nane mwaka wa 2010, wizara ya kilimo ya Indonesia ilianza mpango wa Merauke Integrated Food and Energy Estate), ambayo ilikuwa na lengo la kubadilisha heka milioni 1.2 za ardhi katika eneo Papua ya kusini sehemu ya Merauke kuwa mashamba. Ilipofika mwaka 2011, wawekezaji 36 tofauti walikwishapata sehemu hiyo na kulima miti, miwa, mahindi na njegere.

Uamuzi unapofanyika, wanavijiji hawahuishwi na hutegwa bila kujali na wawekezaji. Ni vizuri kanisa kufahamisha waumini wake juu ya hali hii. UEM ilipozuru Sumatra, ilijionea hali hii. Makampuni ya madini, kilimo na viwanda vya karatasi yalikuwa yakiwadanganya watu na kuwanyang'anya ardhi yao kwa namna hii. Makampuni ya wawekezaji yanawashawishi viongozi wa vijiji ambao pia hutumika kuwashawishi wanavijiji juu ya mambo wawekezaji wanayoyataka.

*Christina Felschen, freelance journalist, Germany*

## Sala

Mwenyezi Mungu uliumba mbingu na dunia kwa ajili yetu, lakini mara nyingi hatuoni umuhimu wa uumbaji wako, badala yake tumeuharibu.

*Umoja wa Makanisa ya Kiinjili (UEM), Mkutano Mkuu wa Mkoa Asia, 2011*

## Mungu mwenye nguvu, Mumbaji wa watu

- K Mungu mwenye nguvu, Mungu wa watu,  
W Wewe ni uhai wa kila kinachoishi,
- K Nguvu inayojaza dunia,  
W Nguvu zinazoleta uhai,
- K Nguvu ziletazo msukumo wa kutengeneza kitu  
kilichovunjika kuwa kizima kwa namna yoyote.
- W Katika Mungu tunajua ukweli kwamba uumbaji  
wake alitupa bure.
- K Wewe ni wimbo unaoimbwa na dunia nzima,  
W Wimbo uletao uhuru leo na hata milele.

## Baraka

Tumekuwa wageni wa Yesu Kristo.  
Tumepokea zawadi nzuri kutoka kwa Mungu.  
Sasa tunaenda majumbani kwetu,  
Kwa majirani zetu na kazini kwetu,  
Tumejitayarisha kuweka maneno ya Bwana Yesu katika  
matendo,  
Ili yaye chumvi ya dunia,  
Ili yatafute haki,  
Ili yalete amani,  
Ili yatunze uumbaji wa Mungu,  
Ili uhai wake urudi.

Wote Asante na amen.

Kimetengenezwa na Umoja wa Makanisa ya Kiinjili Umoja waa Makanisa katika bara tatu  
 Rudolfstrasse 137 · D-42285 Wuppertal · Ujerumani  
 Simu +49 (0) 202 89004 -0 · Faksi +49 (0) 202 89004 -179  
 jpic@vemission.org · www.vemission.org  
 Mhariri Brunhild von Local (editor-in-chief), Christian Sandner  
 Kimetafsiliwa na Mela Hayati Badruddin  
 Picha Christina Felschen, Christian Sandner  
 Jalada limebuniwa na Juan González  
 Kimebuniwa na MediaCompany GmbH, Bonn  
 Nakala 300  
 Chapa Druckerei Kliewer, Siegburg  
 © Muungano wa misioni ya Kiinjili Novembra 2012



Rudolfstrasse 137  
 D-42285 Wuppertal  
 Fon +49 (0) 202 89004 -135  
 Fax +49 (0) 202 89004-179  
 info@vemission.org  
 www.vemission.org

# “Uhusiano wa Hali ya Hewa na Maisha ya Kiroho”

**“Uhusiano wa Hali ya Hewa na Maisha ya Kiroho”** ni mkusanyiko wa habari mbalimbali kuhusu mazingira na haki za binadamu ambao unanaunganisha nyimbo, vifungu vya biblia, madhibitisho, simulizi na sala. Mkusanyiko huu umetayarishwa kwa ajili ya kusaidia sharika zinazohusiana na UEM na pia kusaidia katika kubadilishana mawazo juu ya hali ya dunia yetu. “Uhusiano wa Hali ya Hewa na Maisha ya Kiroho” inajaribu kusaidia katika kusukuma namna nzuri ya kuleta mafanikio kwa kubadilishana mawazo juu ya hali zetu za kiroho katika makanisa yetu.

Kitu kimoja kiko wazi: tunaweza kufanya vizuri katika jambo hili iwapo kila mmoja atatoa mawazo yake juu ya »Uhusiano wa Hali ya Hewa na Maisha ya Kiroho«. Kila mmoja anakaribishwa kutoa hoja, nyimbo, maneno ya Biblia, madhibitisho, simulizi, na sala juu ya haki ya hali ya hewa, utunzaji wa mazingira na haki za binadamu katika sharika zetu, makanisa na majimbo. Iwapo utapenda kutoa mawazo yako ya »kiroho« juu ya uumbaji na uhusiano wake na hali ya hewa, utunzaji wa mazingira na haki za binadamu kwa kushirikiana na wajumbe ndani YA UEM, tuma mawazo yako katika kitengo cha Haki, Amani, na Kuheshimu uumbaji wa Mungu kwa kutumia anuani ya baruapepe: jpic@vemission.org. Mawazo yako yatawekwa katika tovuti ya UEM ([www.vemission.org/climatespirituality](http://www.vemission.org/climatespirituality)). Katika tovuti hii, watu wengine ambao ni wajumbe wa UEM wanaweza kuwa na uhuru wa



Against land grabs. For human rights

Department for Justice, Peace and the Integrity of Creation  
Rudolfstrasse 137 · 42285 Wuppertal · Germany  
www.vemission.org



kuyatumia. Tovuti ya UEM inatoa nafasi ya kutoa mawazo haya kwa watu na kuruhusu upatikanaji wake. Kwa namna hii, mawazo yote ambayo yamekusanya juu ya jambo hili yapo tayari katika tuvuti iliyopo hapo juu. Kwa hiyo kuna nafasi kubwa zaidi ya kuweka mawazo kutoka kwa yeoyote ambaye anapenda kutoa ujumbe wake. Mnakaribishwa!

Tunategemea mchango wa mawazo kutoka kwenu!

“Uhusiano wa Hali ya Hewa na Maisha ya Kiroho” itakua pia katika lugha za Kijerumani, Kingereza na Kifaransa mwishoni mwa mwaka.”